twiga cement

HEIDELBERGCEMENT Group

# TAARIFA YA MWAKA YA MAHESABU 2006

*MAADHIMISHO YA MIAKA AROBAINI*

**1966 - 2006**













Embassy



## *Taarifa ya* **Mwenyekiti**

Kampuni ya saruji ya Tanzania Imepata mafanikio ya kuridhisha mwaka 2006. Kulinganisha na kipindi cha mwaka uliotangulia, mauzo yaliongezeka kwa asilimia 16 na faida iliongezeka kwa asilimia 26 hadi kufikia TZS 19.5 bilioni.

Ingawa ukuaji wa soko la saruji uliathiriwa na matukio mbalimbali hasa ukame na matatizo ya ugavi wa umeme kampuni ilifaulu kutetea nafasi yake katika soko la Dar es Salaam ikiwa inaongoza katika soko hili muhimu. Kuendelea kutoa kipaumbele kwa mahitaji ya wateja wetu, ubora wa bidhaa, ufanisi katika uendeshaji na udhibiti wa gharama ndio sababu la ongezeko la faida. Kuendesha shughuli za kiwanda wakati wa mgao wa umeme, miundombinu duni ya usafirishaji na shilingi kushuka thamani ilikuwa changamoto kwa kampuni. Matukio hayo yalikuwa na athari katika uzalishaji na udhibiti wa gharama.

**Mwaliko wa Umma kununua hisa za kampuni**

Mwaliko wa kwanza wa umma kununua asilimia 30 ya hisa za kampuni zilizokuwa zinamilikiwa na serikali ya Tanzania ulikamilika kwa mafanikio mwezi Septemba 2006. Mwaliko ulizidi hisa zilizokuwa zinauzwa mara tatu na hisa ya kampuni ndiyo inayofayiwa biashara sana katika Soko la hisa la Dar-es Salaam tangu isajiliwe Septemba 29.

**Matarajio**

Kadri hali ya uchumi wa nchi inavyoboreka, mahitaji ya saruji yanatarajiwa kuongezeka sana mwaka 2007 na miaka ijayo. Kampuni imeidhinishiwa mradi wa zaidi ya dola za kimarekani 100 kujengea mtambo wa kisasa wenye uwezo wa kuzalisha tani 2,500 kwa siku. Mradi umeanza rasmi tarehe 1 Machi 2007 na unatarajiwa kuanza uzalishaji kwa awamu mwaka 2008 na 2009.

Mradi huu wa upanuzi utaifanya kampuni iongoze kwa kuzalisha saruji nchini ukiwa pia na teknolojia ya kisasa na pia ukiwa inajali mazingira.

**Shukurani**

Bodi ya Wakurugezi inapenda kutoa shukurani kwa wadau wote kwa michango yao mwaka uliopita na inatarajia ushirikiano utaendelea miaka ijayo pia.

**Gawio**

Kutokana na mahitaji ya fedha kwa ajili ya mradi wa upanuzi ulioidhinishwa, Bodi ya wakurugenzi inapendekeza gawio la T Sh. 28 kwa kila hisa. Gawio hili ni sawa na asilimia 26 ya faida iliyopatikana.

Usajili wa wanachama utafungwa tarehe 16 Mei 2007. Siku ya mwisho ya biashara pamoja na gawio itakuwa tarehe 10 Mei 2007. Gawio litalipwa tarehe au karibia tarehe 31 Mei 2007.

Jean-Marc Junon
**Mwenyekiti wa Bodi**





## *Taarifa ya* **Mkurugenzi Mkuu**

Mwaka wa fedha wa 2006 umekuwa mwaka mwingine wa mafanikio kwa Kampuni ya Saruji Tanzania.

**Uchumi**

Tanzania imeshuhudia ongezeko kubwa la pato halisi la taifa tangu mwanzo wa milenia, hadi kufikia wastani wa takriban asilimia 7 katika kipindi cha 2002-04 kukiwa pia na hali ya mfumuko wa bei mdogo. Ukame hasa katika maeneo ya kaskazini mwa Tanzania katika mwaka 2005-06 pamoja na tatizo kubwa la umeme viliathiri ukuaji wa uchumi na kukifikisha chini ya matarajio ya serikali.

**Mauzo na Maendeleo ya Soko**

Kwa ujumla soko la saruji nchini Tanzania limeongezeka kufikia makisio ya tani 1,480,000. Kati ya kiasi hicho tani 1,450,000 zilizalishwa humu nchini. Soko lilikuwa kwa kiwango kizuri cha 4.8%.

Ongezeko la soko kwa maeneo mbalimbali halikuwa na uwiano. Mauzo ya saruji katika eneo la kusini yaliongezeka kwa kiasi kikubwa cha 23% ikifuatiwa na eneo la Unguja na kaskazini yalikoongezeka kwa 11%. Dar es Salaam mauzo yaliongezeka kwa 7% na ukanda wa kati kwa 5%, ambapo mauzo katika ukanda wa ziwa yalipungua kwa zaidi ya 40%.

**Uzalishaji na Mradi wa Upanuzi wa Kiwanda**

Kampuni ilianza kuendeleza maeneo mapya ya kuchimba, pamoja na kuchimba mchanga wa udongo wa mfinyanzi kwa majaribio katika matayarisho ya mchanganyiko ghafi. Pia imekuwa ikitumia mabwawa kukusanyia maji ya mvua yanayotumika kupunguza vumbi kiwandani na barabarani.

Kufuatia mwaka wa mafanikio na ziara iliyofanywa na Bwana Dr. Bernd Scheifele,rais wa Heidelberg Cement kwa Muheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya muungano wa Tanzania kampuni iliamua kuwekeza zaidi ya dola za Marekani milioni 100. Pesa hizo zitatumika kwa kuweka mtambo mpya wa kutengeneza saruji na upanuzi wa kiwanda katika miaka miwili ijayo.

**Wafanyakazi**

Mwaka huu wafanyakazi kumi waliacha kazi. Wafanyakazi wengi walipatiwa mafunzo kwenye taasisi mbalimbali nje ya kiwanda na wengine walipata mfunzo humuhumu kiwandani. Mafunzo yalikuwa katika maeneo ya sheria za kazi, uhandisi majengo na ubora wa bidhaa. hakukua na ajali mbaya kiwandani, na ajali ndogo ndogo zilizotokea zilishughulikiwa maramoja.

**Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii**

Kampuni ilitoa msaada wa tani 470 za saruji katika uwajibikaji kwa jamii. Msaada wote huu ulielekezwa katika miradi ya ujenzi wa shule za sekondari ambayo ni eneo lililopewa umuhimu mkubwa na serikali ya awamu ya nne katika azma yake ya kuongeza idadi ya wanaokwenda sekondari baada ya shule ya msingi.

**Matarajio ya 2007**

Mwaka 2007 utatoa changamoto kwa namna nyingi. Pamoja na uhafifu wa umeme ambao utaendelea kuleta matatizo ya uendeshaji na gharama, utekelezaji wa upanuzi utanza katikati ya mwaka 2007.

Hata hivyo uongozi wa kampuni unaamini kwamba mwaka ulio mbele yetu utakuwa mwaka mwingine wa mafanikio kwa wadau wote wa kampuni.

Klaus Hvassing
**Mkurugenzi Mtendaji**



| TARRIFA YA MAPATO | 2006<br>Tzs'000 | 2005<br>Tzs'000 |
|---|---|---|
| Mapato | 80,203,239 | 69,038,626 |
| Gharama za Mauzo | 37,192,018 | 35,848,135 |
| **Faida Ghafi** | **43,011,222** | **33,190,490** |
| Mapato Mengineyo | (115,134) | (995,940) |
| Riba | (290,721) | (895) |
| Mauzo ya mali ya kudumu | (9,328) | (22,262) |
| Gharama za Wafanyakazi | 1,584,729 | 2,160,388 |
| Gharama za Mauzo na Uongozi | 5,523,839 | 5,406,066 |
| Uchakavu wa mali ya kudumu | 2,768,886 | 2,581,541 |
| Gharama Nyinginezo | 901,298 | 481,561 |
| Punguzo la thamani ya vipuli | 4,105,855 | - |
| Hasara ya ubadilishaji fedha | 264,192 | 341,346 |
| Gharama ya usimamizi wa fedha | 345,275 | 828,524 |
| | **15,078,890** | **10,780,329** |
| **Faida ya biashara** | **27,932,331** | **22,410,161** |
| Kodi | 8,432,293 | 6,781,775 |
| **Faida baada ya kodi** | **19,500,038** | **15,628,386** |
| **Faida kwa kila hisa** | **108.38** | **86.86** |

| MIZANIA | 2006<br>Tzs'000 | 2005<br>Tzs'000 |
|---|---|---|
| **MALI** | | |
| **Mtaji na akiba** | | |
| Mali isiyohamishika, Mitambo na vifaa | 29,172,977 | 26,703,616 |
| Mali isiyoshikika | 28,408 | 69,046 |
| Ardhi | 209,622 | 211,126 |
| Wadaiwa wa muda mrefu | - | 34,901 |
| | **29,411,008** | **27,018,688** |
| **Mali za muda mfupi** | | |
| Leasehold land | 5,440 | 5,440 |
| Akiba ya fedha | 8,149,852 | 10,239,222 |
| Mali ghafi, vipuli na mali za kuuzwa | 13,177,260 | 11,100,990 |
| Wadaiwa wa biashara | 2,510,930 | 2,027,030 |
| Wadaiwa wengineo | 14,630,972 | 1,636,071 |
| Madai ya marejesho ya kodi | 953,369 | - |
| | **39,427,823** | **25,008,753** |
| **JUMLA YA MALI** | **68,838,831** | **52,027,442** |
| **MTAJI NA DHIMA** | | |
| Mtaji na akiba ya faida | | |
| Hisa zilizotolewa | 3,598,462 | 3,598,462 |
| Faida iliyobakizwa | 50,218,032 | 33,842,681 |
| | **53,816,494** | **37,441,143** |
| **Madeni ya Muda Mrefu** | | |
| Tathmini ya kodi isiyosogezwa mbele | 7,180,050 | 7,177,783 |
| Mikopo ya Muda mrefu | 629,548 | 679,912 |
| Matengo ya mafao ya wafanyakazi | 481,985 | 408,495 |
| | **8,291,583** | **8,266,189** |
| **Madeni ya muda mfupi** | | |
| Sehemu ya madeni ya muda mrefu yanayoiva | 85,464 | 81,477 |
| Madeni ya kibiashara na mengineyo | 6,645,290 | 5,776,716 |
| Deni la kodi | - | 461,917 |
| | **6,730,754** | **6,320,109** |
| **JUMLA YA MTAJI NA DHIMA** | **68,838,831** | **52,027,442** |

Taarifa hii ya Mahesabu imeidhinishwa na Bodi ya wakurugenzi tarehe _______________2007 na kutiwa sahihi kwa niaba yao na:

Jina: ______________________ Cheo: ____________________ Sahihi: __________________

Jina: ______________________ Cheo: ____________________ Sahihi: __________________

| TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI | SHARE CAPITAL<br>Tzs'000 | RETAINED EARNINGS<br>Tzs'000 | PROPOSED DIVIDEND<br>Tzs'000 | TOTAL<br>Tzs'000 |
|---|---|---|---|---|
| Mnamo Januari 1, 2006 | 3,598,462 | 31,342,681 | 2,500,000 | 37,441,143 |
| Gawio lililopendekezwa | - | - | - | - |
| Gawiola ziada lililopendekezwa | - | (624,688) | 624,688 | |
| Gawio lililolipwa | - | 0 | (3,124,688) | (3,124,688) |
| Faida ya mwaka 2006 | - | 19,500,038 | - | 19,500,038 |
| **Mnamo Decemba 31, 2006** | **3,598,462** | **50,218,032** | **-** | **53,816,494** |
| Mnamo Januari 1, 2005 | 3,598,462 | 18,214,295 | 1,800,098 | 23,612,855 |
| Gawio lililopendekezwa | - | (2,500,000) | 2,500,000 | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (1,800,098) | (1,800,098) |
| Faida ya mwaka 2005 | 15,628,386 | - | 15,628,386 | |
| **Mnamo Decemba 31, 2005** | **3,598,462** | **31,342,681** | **2,500,000** | **37,441,143** |

# *Taarifa ya* **Mahesabu**

## *mwisho wa mwaka 31 Disemba 2006*

| MTIRIRIKO WA FEDHA | Note | 2006<br>Tzs'000 | 2005<br>Tzs'000 |
|---|---|---|---|
| **Fedha zinazotokana na shughuli za uendeshaji** | | | |
| Faida kabla ya kodi | | 27,932,331 | 22,410,161 |
| ***Marekebisho ya:*** | | | |
| Uchakavu wa mali ya kudumu | | 2,768,886 | 2,581,541 |
| Riba | | 345,275 | 828,524 |
| Faida inayotokana na mauzo ya mali za kudumu | | (9,328) | (22,262) |
| **Fedha zinazotokana na biashara** | | **31,037,164** | **25,797,965** |
| **Fedha zinazotokana na biashara** | | | |
| Ongezeko la bidhaa | | (2,076,270) | (583,153) |
| Ongezeko la Wadaiwa wa biashara | | (483,900) | (14,432) |
| Ongezeko/(kupungua) wadaiwa wengine wa uendeshaji | | (12,994,901) | 372,202 |
| Kupungua kwa wadaiwa wa muda mrefu | | 34,901 | 52,505 |
| Matengo ya mafao ya wafanyakazi | | 73,491 | 408,495 |
| Ongezeko/(punguzo) la wadai | | 868,575 | (2,302,105) |
| **Fedha zinazotokana na uendeshaji** | | **16,459,059** | **23,731,477** |
| Kodi ya mapato iliyolipwa | | (9,845,312) | (4,401,884) |
| Riba iliyolipwa | | (341,287) | (845,155) |
| **Fedha halisi zinazotokana na shughuli za uendeshaji** | | **6,272,460** | **18,484,438** |
| **Fedha iliyotumika kwenye vitega uchumi** | | | |
| Mauzo ya mali ya kudumu | | 223,099 | 23,330 |
| Endelezo la ujenzi wa mali za kudumu | | (13,625,712) | (966,258) |
| Ununuzi wa mali zisizoshikika | | (15,461) | (97,477) |
| Manunuzi ya mali ya kudumu | | 8,231,295 | (2,060,883) |
| **Fedha halisi iliyotumika kwenye vitega uchumi** | | **(5,186,778)** | **(3,101,288)** |
| **Fedha iliyotumika kwenye shughuli za fedha** | | | |
| Gawio lililolipwa | | (3,124,688) | (1,800,098) |
| Malipo ya wadai wa muda mrefu | | (50,364) | (50,364) |
| **Fedha halisi iliyotumika kwenye shughuli za fedha** | | **(3,175,051)** | **(1,850,462)** |
| **Mabadiliko halisi ya fedha** | | **(2,089,369)** | **13,532,68** |
| Fedha iliyokuwepo Januari 01 | | 10,239,222 | (3,293,466) |
| **Fedha iliyokuwepo Desemba 31** | | **8,149,852** | **10,239,222** |

**PUNGUZO LA THAMANI YA VIPULI – TZS 4,105,855,000**

HeidelbergCement imeanzisha sera mpya ya kuthamini vipuli kuanzia mwaka 2006. Sera hii itatekelezwa na kampuni tanzu zote ikiwemo Kampuni ya Saruji Tanzania. Madhumuni ya sera hii ni ni kuweka ukomo wa tahadhari ya mizania kwa kufanya tathmini ya vipuli kulingana na Viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa taarifa za fedha (IFRS), hususan Viwango vya kimataifa vya utunzaji hesabu na. 2 (IAS 2) Sera hii imetumika kwa mara ya kwanza katika mahesabu ya Kampuni ya Saruji Tanzania na imesababisha punguzo la thamani ya vipuli kiasi cha TZS 4,105,855,000 ambayo imeonyeshwa kama gharama isiyotokana na uendeshaji na isiyotokea kila mwaka.

**WADAIWA WENGINE WATOKANAO NA UENDESHAJI TZS 14,630,972,000**

Kiasi hicho kinajumuisha fedha za kitanzania zinazolingana na dola za kimarekani 10,800,000 walizolipwa Scancem International ANS kwa ajili ya malipo ya awali kuhusiana na ununuzi wa mitambo ya mradi wa upanuzi. Mradi wa upanuzi unakadiriwa kugharimu dola za Marekani 108,000,000 utakapokamilika na malipo ya awali mkataba ukitiwa saini ni asilimia 10 ya gharama iliyokadiriwa.


LINDI

## *Fomu ya* **Mwakilishi**

Kwa matumizi kwenye Mkutana Mkuu wa mwaka wa Tanzania Portland Cement Company Ltd

Mimi/ Sisi ____________________________________________________________

wa S. L. P.______________________ nikiwa mwanachama/wanachama wa Kampuni ya

Tanzania Portland Cement Company Limited Namchagua

____________________________________________________________________________

wa S. L. P ___________________________________________________________________

kama mwakilishi wangu/ wawakilishi/ wetu kupiga kura kwa ajili yangu/yetu na kwa niaba yangu/yetu katika Mkutano Mkuu wa Mwaka utakaofanyika; Zanzibar Room Kilimanjaro Kempinski, Dar-es-salaam, Tarehe: 12. 04. 2007 Saa: 8:30 Mchana. Kama shahidi saini yangu/zetu leo.

Sahii: ____________________________ Tarehe: ____________________________

**Zingatia Yafuatayo:**

1. Ikiwa mteuzi ni shirika au kampuni,fomu hii ni lazima iwe na muhuri wa moto wa kampuni husika na ipitishwe kwa maafisa wa kampuni, wakili au kwa mtu aliyehidhinishwa kusaini nyalaka kwa niaba ya kampuni.
2. Ikiwa hisa zinamilikiwa na zaidi ya mtu mmoja, sahihi ya mwanahisa mmoja inakubalika endapo majina ya wamiliki wote wa hisa yamehorodheshwa kwenye fomu ya uwakilishi.
3. Ili ikubalike, fomu ya uwakilishi inapaswa iwe imejazwa na kufikishwa kwa wakala wetu CAD Securities Limited ndani ya masaa 48 kabla ya muda uliopagwa kwa ajili ya mkutano au kuahirishwa kwa mkutano, na lazima isainiwe na mwanasheria au mamlaka yeyote husika. Kujazwa na kurudishwa kwa fomu hakumzuhii mwanachama kuhudhuria na kuchagua kama anataka kufanya hivyo.

**Fomu irudishwe:**

CAD Securities Limited
3rd Floor
Mwalimu Nyerere Pension Tower
Bibi Titi/ Morogoro Road
P. O. Box 23226
Dar-es-salaam
Tel: 2123030
Fax: 2127622
Email: info@cadsecurities.com